ADVANCE FAMILY PLANNING

# JE, MASKINI WANAFIKIWA?

## Uchambuzi waonyesha kuongezeka kwa maskini wasiopata huduma za uzazi wa mpango Tanzania .....

### UTANGULIZI:

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua kwamba Uzazi wa Mpango ni swala la kiuchumi na lenye kupewa kipaumbele katika juhudi za kukabiliana na umaskini. Katika Mkakati wake wa kupunguza umaskini (MKUKUTA II 2010-2015), serikali imeweka lengo la kupunguza wastani wa uzazi kwa kila mwanamke aliye katika umri wa kuzaa kutoka 5.4 hadi 5.0; vifo vya wamama vinavyo husiana na uzazi kutoka 454 hadi 265 kwa kila vizazi hai 100,000; na vifo vya watoto wachanga kutoka 26 hadi 19 kwa kila vizazi hai 1,000 ifikapo mwaka 2015. Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya III, Julai 2009 na Mpango wa Taifa wa Kutekeleza Huduma za Uzazi wa Mpango (NFP CIP 2010-2015) inaonyesha dhamira ya serikali katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma za uzazi wa mpango zinaongezeka na kupatikana kwa watanzania wote. Kwa mfano, mkakati wa uzazi wa mpango unaonyesha lengo la kitaifa la upatikanaji wa huduma za uzazi wa mpango kwa 60% kwa wanawake wote ifikapo mwaka 2015. Uchambuzi kuhusu watu wanaopata huduma za uzazi wa mpango (kutokana na taarifa za utafiti (DHS) za 2010) ulifanywa pamoja na makisio ya ongezeko la watumiaji wa huduma za uzazi wa mpango hadi 2015. Matokeo yanaonyesha kusuasua na uwezekano mkubwa wa kutofikia malengo kama hali ya mwenendo wa sasa itaendelea.

### MATUMIZI YA UZAZI WA MPANGO YAMEONGEZEKA KWA WATU WA KIPATO CHA JUU:

Taarifa zinaonyesha kwamba matumizi ya vifaa vya uzazi wa mpango (kwa njia za aina zote) katika miaka 20 iliyopita yameongezeka kwa zaidi ya mara tatu kutoka 10% mwaka 1991 hadi 34% mwaka 2010. Ongezeko hili linatia moyo. Hata hivyo, zaidi ya mara mbili ya matumizi hayo ni kwa wanawake wenye kipato cha juu (38%) yakilinganishwa na yale ya wanawake walio maskini zaidi (19%.). Angalia Kielelezo 1.

Wastani wa uzazi kwa kila mwanamke vijijini ni 6.1 wakati ya mijini ni 3.7, ikimaanisha kwamba wakazi wa vijijini ndio wanaoinua kiwango cha uzazi nchini. Kwa hiyo, mipango ya kupunguza kiwango cha uzazi lazima itilie maanani kuwafikia wanawake wa vijijini na walio maskini zaidi, ndipo kiwango cha uzazi kitaweza kupungua kwa namna ya kuridhisha na kuiweka nchi katika nafasi nzuri ya kutimiza malengo yake ya kitaifa ifikapo 2015.

**Kielelezo 1: Matajiri wanapata huduma za uzazi wa mpango maradufu**




### HUDUMA ZA UZAZI WA MPANGO: NI NANI WANAOZIPATA?:

Kielelezo namba 2 kinaonyesha kuongezeka kwa akina mama masikini wanaotaka kutumia huduma ya uzazi wa mpango lakini hawapati fursa hiyo. Mwaka 2004 wanawake maskini 24 kati ya mia walikuwa

[1] Tathmini ya hali ya jamii, uchumi na idadi ya watumiaji wa huduma za uzazi wa mpango kwenye sekta za umma na binafsi

ADVANCE FAMILY PLANNING

wanahitaji huduma za uzazi wa mpango lakini hawakupata. Kiwango hicho kikiongezeka mpaka 30 kati ya mia miaka sita tu baadae. Wakati huo, wanawake wenye uwezo kiuchumi 16 kati ya mia walitamani lakini hawakupata huduma za uzazi wa mpango. Kiasi hiki kilipungua mpaka 15 kati ya mia mwaka 2010. Hii inamaanisha kwamba idadi ya wanawake walio maskini zaidi wanaohitaji kutumia huduma za uzazi wa mpango ni kubwa na inaongezeka lakini hawapati huduma hizo.

Zaidi ya hapo, hii inaonyesha kwamba kunapokuwa na ongezeko la matumizi ya huduma hizi miongoni mwa wanawake wenye vipato vya juu, matumizi ya huduma hizo kwa wanawake maskini zaidi yanapungua.

**Kielelezo 2: Hitaji lisilokidhiwa kwa kuzingatia hali ya kipato**




## JE, TANZANIA ITAFIKIA MALENGO YAKE YA CPR YA 60% IFIKAPO MWAKA 2015?:

**La hasha!** Uchambuzi unaonyesha kuwa kama Tanzania itaendelea na juhudi kama ilivyo sasa (Kielelezo 3) itaweza kufikia CPR ya 41% tu kwa wanawake wanandoa badala ya 60%.

Wakati tathmini hii inaonyesha kuwa itakuwa vigumu kufikia CPR ya 60% kwa wanawake wanandoa, itakuwa vigumu zaidi kwa wanawake wote walio katika umri wa kuzaa. Kwa kundi hili la wanawake ambalo CPR yao ilikuwa CPR 29% mwaka 2010 na kwa kuzingatia mwenendo wa sasa, inakadiriwa kwamba CPR itakuwa 34% ifikapo mwaka 2015.

**Kilelezo3: CPR kwa wanawake wanandoa wote 1992-2015**




## NI HATUA GANI ZA KISERA AMBAZO SERIKALI INAWEZA KUCHUKUA?:

1. Simamia utekelezaji wa sera inayowahakikishia wanawake maskini wa vijijini kupata huduma za uzazi wa mpango,
2. Toa agizo kwa halmashauri zote kuweka huduma za uzazi wa mpango kuwa kipaumbele katika mipango yao ya maendeleo na bajeti kwa kutumia PlanRep (chombo au mfumo wa kutengenezea mipango na bajeti),
3. Serikali ihimize huduma za uzazi wa mpango za kuwafikia watu walipo kwa kupitia mifumo ya kijamii

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

Policy Advocacy Department
Human Development Trust Director
Email: advocacy@hdt.or.tz

Program Director
Advance Family Planning
Email: halima.shariff@jhuccp.org

JOHNS HOPKINS BLOOMBERG SCHOOL of PUBLIC HEALTH
Bill and Melinda Gates Institute for Population and Reproductive Health
AFP ADVANCE FAMILY PLANNING